



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA



TANGAZO

MAFUNZO YA KUPIGA MSASA WAKALIMANI KWA VITENDO

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) linapenda kuufahamisha umma kuwa litatoa mafunzo ya msasa kwa wakalimani kwa vitendo kwa kutumia vifaa vyta kisasa vya Ukalimani kuanzia tarehe 03 hadi 14 Aprili 2023, saa 8:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.

Mafunzo hayo yatatolewa katika ukumbi wa Ukalimani uliopo katika ofisi za Baraza la Kiswahili la Taifa, Kijitonyama - Makumbusho, Dar es Salaam.

Wakalimani wote wa Makanisani, Misikitini na nyuga mbalimbali mnakaribishwa.

Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0734 156 883

Limetolewa na:

Kitengo cha Masoko na Uhusiano na Umma

Baraza la Kiswahili la Taifa.

BARABARA YA ALI HASSAN MWINYI, KITALU NA. 45 B, KIWANJA NA. 75-78, KIJITONYAMA,
SANDUKU LA POSTA 4766, DAR ES SALAAM.

Simu ya Kawaida: 255 022 2762213, Simu ya K/Mtendaji: 255 022 2762243 Baruapepe: km@bakita.go.tz
Tovuti: www.bakita.go.tz